

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA TATU**

**KIKAO CHA TATU**

**02 APRILI, 2026**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA TATU

#### KIKAO CHA TATU – TAREHE 02 APRILI, 2026

#### I. DUA:

#### II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

##### WAZIRI MKUU:

Taarifa ya Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na Nyongeza zake yaliyochapishwa tangu Mkutano wa Bunge uliopita kama ifuatavyo:-

1. Toleo Na. 04 la tarehe 23 Januari, 2026;
2. Toleo Na. 05 la tarehe 30 Januari, 2026;
3. Toleo Na. 06 la tarehe 06 Februari, 2026;
4. Toleo Na. 07 la tarehe 13 Februari, 2026;
5. Toleo Na. 08 la tarehe 20 Februari, 2026;
6. Toleo Na. 09 la tarehe 27 Februari, 2026;
7. Toleo Na. 10 la tarehe 06 Machi, 2026;
8. Toleo Na. 11 la tarehe 13 Machi, 2026; na
9. Toleo Na. 12 la tarehe 20 Machi, 2026.

#### III. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

#### **IV. MASWALI YA KAWAIDA:**

##### **OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):**

##### **11. MHESHIMIWA ENG. CHACHA MWITA WAMBURA (GEITA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga na kukarabati mitaro katika Mitaa ya Mbugani na Kivukoni Geita ili kupunguza athari za mafuriko.

##### **12. MHESHIMIWA JUMA MUSTAFA KAWAMBA (IGALULA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza ujenzi wa Daraja la Loya ili liweze kupitika muda wote na kuruhusu shughuli za kijamii.

##### **13. MHESHIMIWA HAWA SUBIRA MWAIFUNGA (TABORA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Barabara ya kutoka Kata ya Uyui, Kakola hadi Ikomwa.

## **OFISI YA RAIS (MAENDELEO YA VIJANA):**

### **14. MHESHIMIWA LATIFA KHAMIS JUWAKALI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Maendeleo ya Vijana):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kukuza Vipaji na Ujuzi wa Vijana wa Tanzania.

### **WIZARA YA NISHATI:**

### **15. MHESHIMIWA TARIMBA GULAM ABBAS (KINONDONI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga Mtambo wa *Refinery* wa kuchakata Mafuta kwa kuwa Mradi wa Bomba la Mafuta toka Uganda unatarajia kuanza.

### **WIZARA YA MAJI:**

### **16. MHESHIMIWA INNOCENT LUGHA BASHUNGWA (KARAGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itapeleka fedha za kukamilisha ujenzi wa Mradi wa Maji wa Kayanga.

**WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

**17. MHESHIMIWA KASSIMU AMARI MBARAKA (TANGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, lini Serikali itafunga viti katika Uwanja wa Mpira wa Mkwakwani - Tanga kwa kuwa viti vimepelekwa na vipo uwanjani.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**18. MHESHIMIWA ASMA ALI MWINYI (WELEZO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali ya Muungano na Zanzibar zina mpango gani wa kuunganisha na kukuza Utalii nchini kwa kuzingatia bajeti, miundombinu na fursa za ajira.

**WIZARA YA UJENZI:**

**19. MHESHIMIWA HAWA MCHAFU CHAKOMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itajenga Daraja litakalounganisha Tarafa ya Mkongo kati ya Kata ya Mkongo na Utete ambayo ni Makao Makuu ya Wilaya Rufiji.

**WIZARA YA KILIMO:**

**20. MHESHIMIWA CLAYTON REVOCATUS CHIPANDO (KIGOMA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kushughulikia Wakandarasi wanaochelewesha Miradi kama Mradi wa Delta ya Mto Luiche.

**V. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI MKUU:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

***(Majadiliano yanaendelea)***

**DODOMA  
02 APRILI, 2026**

**BARAKA I. LEONARD  
KATIBU WA BUNGE**